



**Mwongozo wa mafunzo kwa wasimamizi
wa ICS kwa ajili ya kufikia viwango vya
kilimohai vya Umoja wa Ulaya (EU)."**



in cooperation with




MAANDALIZI YA MAARIFA HAYA

- Nakala hii ni tafsiri ya kiswahili ya mwongozo wa mafunzo ya Mfumo wa Udhibit wa Ndani (ICS) uliotengenezwa awali kwa lugha ya Kiingereza kupitia ushirikiano wa shirika la kilimohai Tanzania (TOAM) na IFOAM – Organics International.
- Mwongozo huo ulishirikisha wadau wa ICS nchini Tanzania kuchangia ujuzi na maarifa ya namna mfumo huu unapaswa kutekelezwa.
- Kupitia mradi wa kitovu cha maarifa Afrika Mashariki (KHEA), TOAM iliweza kutafsiri mwongozo wa mafunzo haya kwa lugha ya Kiswahili ili kurahisisha matumizi yake kwa wadau mbali mbali wa mnyororo wa thamani. iliunga mkono tafsiri ya mwongozo huu kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili, kama sehemu ya kuwezesha upatikanaji na usambazaji wa maarifa kuhusu ICS.


UTANGULIZI KUHUSU MAARIFA HAYA

- Mwongozo huu wa Mafunzo ya Mfumo wa Udhhibiti wa ndani (ICS) ni sehemu ya mfululizo wa nyenzo za mafunzo unaojumuisha seti 3, zilizolenga kuwajengea washiriki uelewa na uwezo wa kutumia Mfumo wa ICS katika Kilimohai.
- Nakala hii imejikita katika moduli Set 2 iliyowalenga vikundi vya wakulima na operetta wengine kulingana na mahitaji ya viwango vya ulaya (EU) ikiwa ni Pamoja na utangulizi kuhusu kikundi cha operetta, kanuni za kuwa mwanachama wa kikundi, na taratibu za kuendesha kikundi cha opereta kwa kufuata misingi ya ICS.

Viashiria vya udhibitishaji wa kikundi.



viashiria vikuuu vya uthibitishaji wa kikundi.



Viashiria vikuu vya udhibitishaji wa kikundi

	Vijitabu	Cheti	mkataba	Mambo mengine ya CB	Maelezo	Muongozo wa ICS	Kumbu kumbu	usajili
wakulima	X	X	X	X	X	X	X	
Wafanya kazi	X		X		X	X	X	
Wakaguzi wa ICS	X		X		X	X	X	
Wasimammizi wa ICS	X		X	X	X	X	X	
Partners	X		X	X	X	X	X	
Kikundi		X		X	X	X	X	X
Chombo cha udhibitishaji		X	X	X				X
Chombo cha udhibitishaji / AB / Comm		X						X

Yaliyomo kwenye mafunzo

Siku ya kwanza

Msisitizo kwa
wakulima na wakaguzi
wa ICS.

Siku ya pili

Msisitizo kwa kikundi

Siku ya tatu

Msisitizo kwenye chombo
cha uthibitishaji




Yaliyomo siku ya Pili: Msisitizo kwa opereta wa kikundi cha ICS.


1. Maelezo ya mahitaji ya kikundi.
2. Kikundi kinaruhusiwa kufanya nini?
3. ICS inaundwaje?

Kundi la Opereta (GoO) ni nini

Kundi la Opereta ni nini?



Kikundi cha opereta ni nini



Kinaundwa na wanachama ambao:

Ni wakulima wa kilimohai.

Chini ya kikomo cha ukubwa/mauzo ya juu (< 5 ha jumla ya ardhi, AU < €25,000 mauzo ya kilimohai)

Wasiozidi 2000

Kimeanzishwa nchini Tanzania na kinatambulika kisheru

Kina mfumo wa udhibiti wa ndani (ICS_

Kina mfumo wa uuzaji wa pamoja

Wanachama watakiwa kuwa karibu kijiografia.

Mwanachama atasijili katika kukindi cha uendeshaji kimoja kwa ajili ya zao flani.

Sifa za wanachama #1: Vipi kuhusu shughuli za maandalizi?



Kikundi cha opereta

Kinaundwa na wakulima



Kifungu cha 36.1 (a) kinafafanua kwamba Kundi la operetta:

- Liwe na wanachama ambao ni wakulima au opereta wanaozalisha mwani au wanyama wa kufuga katika maji na ambao pia wanaweza kushiriki katika usindikaji, utayarishaji au uwekaji sokoni wa chakula au malisho (shughuli za maadalizi)



Kuosha mbogamboga.



Kupanga mboga mboga.



Kukausha kahawa.



kuvua maganda ya karanga/karanga kubwa.

Ustahiki wa wanachama #1: Vipi kuhusu maandalizi?



Kikundi cha opereta

Kimeundwa na wakulima.



Kifungu cha 36.1 (a) kinafafanua kwamba Kundi la Waendeshaji lita... Liwe na wanachama ambao ni wakulima au waendeshaji wanaozalisha mwani au wanyama wa kufuga katika maji na ambao pia wanaweza kushiriki katika usindikaji, utayarishaji au uwekaji sokoni wa chakula au malisho.

Uhifadhi

uchakataji

ufungashaji

Shughuli yoyote juu ya bidhaa ambazo hazijachakatwa ambayo haibadilishi bidhaa za awali

Kuweka lebo kwa bidhaa za kilimohai.



Kuosha mboga



Kuchambua mboga




Kukausha kahawa



Kutoa Maganda

Shughuli za maandalizi katika kikundi cha opereta.



Mashirika yote ya wakulima hufanya angalau baadhi ya shughuli za maandalizi baada ya kukusanya bidhaa kutoka kwa **wanachama**, mfano: kuchambua, kupanga madaraja, kuchanganya, kufungasha, na wakati mwingine pia "kuchakata" (k.m. kukausha bidhaa) kama sehemu ya mfumo wao wa pamoja wa uuzaji.

Hata hivyo, ufafanuzi katika Kifungu cha 36.1 unasema tu kwamba wanachama ni wakulima (...) ambao kwa kuongezea wanaweza kushiriki katika maandalizi na usindikaji.

Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara kwenye Tume ya EU: Je, kundi la waendeshaaji linaweza kufanya shughuli za uchakataji kwenye bidhaa wanazopokea kutoka kwa wanachama wake?

Ndiyo. Kundi la waendeshaaji walioidhinishwa kama la kilimohai katika EU, au kundi la waendeshaaji walioidhinishwa kama la kilimohai katika nchi nyingine wanaweza kufanya shughuli yoyote, ikiwa ni pamoja na "uchakataji", chini ya uthibitisho wa kundi.



Stahiki za wanachama #1: Vipi kuhusu wanachama.



Maandalizi ya shambani



Kituo kikuu
cha
kukusanyia

Kituo kikuu
cha
kukusanyia



Maandalizi ya shambani katika
vituo vya mmoja (au zaidi) wa
wanachama





“Stahiki za wanachama #2: Jinsi ya kubaini mauzo ya kila mwaka ya uzalishaji wa kilimohai?”



Je, ni kiasi gani cha mauzo ya mwanachama kutokana na uzalishaji wa kilimohai?

Thamani ya kila mwaka ya mauzo ya bidhaa za kilimohai ambazo mwanachama ameua kwenye kikundi.

- Jumla ya mauzo yaliyokusanywa kwa mwaka wa hesabu (mwaka uliopita)
- Ikizingatia bei ya bidhaa kama ilivyolipwa kihalisi kwa mwanachama
- Ruzuku hazihesabiwi kama mauzo

Vipi kuhusu mabadiliko makubwa au ya ghafla katika kiasi cha mauzo, bei, na viwango vya kubadilisha fedha?

ICS itaweka kanuni na taratibu za kuhakikisha sifa za wanachama; ambazo zitapitiwa na kuidhinishwa na CB.

Ushauri wa ziada kutoka IFOAM:

- Lengo = Uendelevu wa uanachama katika GoO: si kujiunga na kujiondoa kila mwaka.
- Kutumia wastani wa kila mwaka wa ubadilishaji wa fedha kwenda Euro ni utaratibu wa kawaida wa EU, kwa mfano, kutumia thamani ya miezi 12 kutoka mfumo wa kubadilisha fedha (kama vile InforEURO).
- Vikundi vinashauriwa kusimamia kwa uangalifu uzingatiaji wa kanuni za kiasi cha mauzo (turnover) na kuzingatia uwiano wa usalama katika uanachama wao.



Ustahiki wa wanachama #3: jinsi ya kutathmini ukubwa wa shamba wa wanachama.

Holding' ya mwanachama ni nini? Je, inamaanisha ardhi ya kilimohai pekee?

Holding = vMashamba yote ya uzalishaji vinavyoendeshwa na mwanachama kwa madhumuni ya kuzalisha mazao ya kilimo, ikiwemo bidhaa kutoka ufugaji wa samaki na ufugaji wa nyuki.“

Mashamba ya kilimo hai pamoja na mashamba yasiyo ya kilimo hai au yaliyopumzishwa kwa ajili ya mzunguko wa mazao.

Vipande vya misitu havihusishwi, isipokuwa vinapotumika kwa uzalishaji wa bidhaa za kilimo hai kama vile ufugaji wa samaki



Vipi kuhusu mashamba makubwa zaidi katika vyama vyetu vya ushirika?

Iwapo shamba lina ukubwa wa zaidi ya hekari 5 (5ha) NA mapato yake kutokana na kilimo hai yanazidi €25,000 kwa mwaka, haliwezi kuwa mwanachama wa GoO.

- Ili kuuza mazao kama ya kilimohai, shamba linahitaji kuthibitishwa kuwa shamba la kilimohai na chombo cha uthibitishaji (CB)
- Mkulima hawezi kubaki kama mwanachama rasmi wa kundi/chombo cha GoO
- ❖ Aidha shamba hilo kubwa huondolewa kwenye uanachama rasmi
- ❖ AU chama cha ushirika huunda chombo kipya cha kisheria cha GoO kwa ajili ya wakulima "wadogo" pekee

Tazama sehemu inayofuata


Eneo lote la ardhi linalosimamiwa na mwanachama' = kipengele cha lazima katika orodha ya wanachama wa GoO. Lazima lisajiliwe na ICS na libaki likisasishwa kwa kila mwanachama.

Stahiki za wanachama #4: Katika vyama vya wakulima vyenye wanachama wasiowakulima wa kilimohai waliowekwa kisheria.

Chama chetu cha ushirika kina wanachama wadogo 300 wanaozalisha kwa njia ya kilimohai na 100 wanaozalisha kwa njia ya kawaida. Tumekuwa na vyeti vya uthibitishi vya EU na NOP kwa miaka 10 sasa. Je, tunaweza kupata cheti cha GoO?

Hapana. Kulingana na tafsiri ya Umoja wa Ulaya (EU), Ibara ya 36.1 inaashiria kuwa ushirika wenye wanachama wa kisheria ambao si wakulima wa kilimohai hauwezi kupata cheti cha GoO. Wanachama wote wa kisheria wa taasisi inayohusika na GoO lazima watimize vigezo stahiki vilivyoainishwa katika Ibara ya 36.1 (yaani, wawe wakulima, wazingatie kanuni za kilimohai, wasivuke mipaka ya juu ya ukubwa au mapato, na wawe katika eneo la karibu kijiografia).

Chama hiki cha ushirika hakiwezi kuthibitishwa kwa ajili ya uzalishaji wa kilimohai, lakini kinaweza kupitia shughuli nyingine .



Kundi (au kikundi kidogo) la wakulima wadogo wa kilimo hai linaweza kupata cheti cha GoO iwapo lina usajili unaotambulika kisheria



Maswali na Majibu ya Tume ya Umoja wa Ulaya: Wanachama wasio wa kilimohai katika Kikundi cha Opereta (GoO)

Swali la 8 la Tume ya Umoja wa Ulaya:

Je, kikundi cha opereta kilichothibitishwa kuwa kilimohai kwa mujibu wa Kanuni (EU) Na. 2018/848 kinaweza kujumuisha wanachama ambao si wakulima wa kilimohai au wanaozalisha mwani au wanyama wa majini?

Jibu:

Hapana. Kikundi cha opereta kinaweza kujumuisha wanachama ambao ni wakulima au opereta wanaozalisha mwani au wanyama wa majini, na ambao wanaweza pia kujihusisha na usindikaji, utayarishaji au uuzaji wa chakula na malisho. Hata hivyo, wakulima au waendeshaji ambao hawazingatii Kanuni (EU) Na. 2018/848 hawawezi kuwa wanachama wa kikundi cha opereta kilichothibitishwa kuwa kilimohai.

Maswali na Majibu ya Tume ya Umoja wa Ulaya: Wanachama wasio wa kilimohai katika Kikundi cha Opereta (GoO)...

Kwanza, Kifungu cha 36(1) cha Kanuni hiyo kinaeleza kuwa kikundi cha waendeshaaji kinapaswa kujumuisha wakulima au waendeshaaji ambao shughuli zao zinaweza kuwa za uzalishaji, usindikaji, utayarishaji au uuzaji wa chakula na malisho.


Pili, masharti yafuatayo ya Kanuni (EU) 2018/848 pia yanahusika:

Kifungu cha 3, aya ya 1(13): “Opereta” ni mtu wa asili au taasisi ya kisheria anayehusika na kuhakikisha uzingatiaji wa Kanuni katika kila hatua ya uzalishaji, utayarishaji na usambazaji ambayo iko chini ya udhibiti wake.

Kifungu cha 36(1)(b): Kikundi cha opereta lazima kiwe na mfumo wa udhibiti wa ndani (ICS) unaojumuisha shughuli na taratibu za udhibiti zilizorekodiwa, ambapo msimamizi au chombo kilichotambuliwa kina jukumu la kuthibitisha uzingatiaji wa Kanuni.


Chanzo: Maswali na Majibu ya Tume ya Umoja wa Ulaya kuhusu kanuni za kilimohai, Toleo la 13, 13 Juni 2023.

Stahiki za wanachama #5: Vipi kuhusu kilimo mchanganyiko cha wakulima?



Je, mkulima anayejihusisha katika uzalishaji wa kilimohai katika sehemu tu ya shamba lake, anaweza kuwa wa kikundi?

Stahiki za wanachama #5: Vipi kuhusu uzalishaji mchanganyiko unaofanywa na wakulima..



Je, mkulima anayejishughulisha na uzalishaji wa kilimohai katika sehemu ya shamba lake anaweza kuwa mwanachama wa kikundi?

Ndio, anaweza.

Katika hali kama hio, ICS itachukua jukumu la kupitia mashamba yote na kuhakikisha utengano kati ya bidhaa na maeneo ya uzalishaji, ikimaanisha kwamba huyu mkulima ana hatari kumbwa zaidi ya kushindwa kukizi vigezo kuliko wakulima wengine

Stahiki za wanachama #6: Je, wakulima wanaweza kuuza kwa wanunuzi zaidi ya mmoja?



Je, wakulima wanaeza kuwa wanachama kwa GoO zaidi ya moja?

Mwanachama wa kundi la opereta anapaswa kujiandikisha katika Kundi moja (GoO) pekee kwa ajili ya bidhaa husika, hata pale ambapo opereta huyo anajishughulisha na shughuli mbalimbali zinazohusiana na bidhaa hiyo.

1. Kwa bidhaa ile ile, mfano kahawa, mkulima **hawezi** kuwa mwanachama katika GoO tofauti.
2. Katika mfano uliotolewa, mkulima anaweza kuwa mwanachama wa GoO moja kwa ajili ya maembe yake ya kilimohai, na nyingine kwa ajili ya kahawa yake.
3. Hata hivyo, hii huleta hatari kubwa zaidi na inahitaji usimamizi makini wa Mfumo wa Udhibiti wa Ndani (ICS).

Wanakikundi wa GoO wanaeza kuuza kwa wanunuuji wengine?

Ni bidhaa zinazouzwa na GoO pekee ndizo zinazothibitishwa kama za kilimo hai..

-Lakini wakulima wadogo kama wajasiriamali wadogo kwa kawaida huuza pia sehemu ya mazao/uzalishaji wao kwa wafanyabiashara wa ndani

-Mauzo yoyote ya aina hiyo HAYATHIBITISHWI kama ya kilimo hai.

-ICS inapaswa kufuatilia mauzo haya mengine na kuyazingatia katika mfumo wa ufuatiliaji wa kundi..

Stahiki za wanachama #7: Jinsi ya kushughulikia mabadiliko katika ngazi ya mwanachama?



Maswali Yanayoulizwa Mara Kwa Mara ya Tume ya EU (10): Je, wakati wanachama wa kundi lililothibitishwa la waendeshaji shughuli hawakidhi tena mahitaji yaliyowekwa katika Ibara ya 36(1)(a) na (b) ya Kanuni (EU) Na. 2018/848, wanaweza kuendelea kuwa wanachama wa kundi hilo la waendeshaji shughuli?

Hapana. Kifungu cha 36(1) cha Kanuni ya 2018/848 kinasema kwamba kila kikundi cha waendeshaji 'kitaundwa tu na wanachama' wanaokidhi, pamoja na masharti mengine, masharti yaliyowekwa katika aya (a) na (b).


Kwa hivyo, mwendeshaji asiyetimiza masharti ya Ibara ya 36(1), vipengele (a) na/au (b) vya Kanuni ya 2018/848 hawezi kuwa mwanachama wa kundi la waendeshaji ikiwa kundi hilo linakusudiwa kudhibitiwa na kuthibitishwa kama kundi la waendeshaji kwa mujibu wa maana ya Ibara ya 36 ya Kanuni (EU) Na. 2018/848..

Kifungu 36.1.(a) ☐ kuwa mkulima au mwendeshaji wa shughuli za mwani/ufugaji wa viumbe vya majini; kuzingatia kanuni za kilimo hai. Kifungu 36.1.(b) ☐ kuwa ndani ya mipaka ya ukubwa wa shamba au mapato ya kilimo hai.

Huwezi kubaki kuwa mwanachama rasmi (kisheria) katika taasisi itakayothibitishwa kama GoO..

Ukubwa wa juu wa kikundi cha opereta.

Kikundi cha opereta.



**Wanachama
wasiozidi 2000 kwa
kila kikundi.**

GoO inaweza kuwa na wanachama wasiozidi 2000

Vikundi vyenye wanachama walioidhinishwa zaidi ya 2000 vitahitaji kuanzisha vikundi vipya kwa ajili ya uidhinishaji wa EU kama GoO.

- Kila kikundi "kipya" cha GoO kitahitaji "kuwa na hadhi ya kisheria" na kiwe na wakulima wa kilimohai au walioko katika kipindi cha mpito pekee
- Haikubaliki kwamba kikundi kipyaa (chenye wanachama chini ya 2000) kutumia cheti cha usajili wa kikundi kikubwa. Kila GoO lazima iwe na hadhi yake binafsi ya kisheria.

Kila GoO itakua na “Usajili wake binafsi kisheria.”



Mwaswali yanayoulizwa mara kwa mara kwa mujinu wa Tume ya Umoja wa Ulaya

Hali ya kisheria binafsi" haifafanuliwi katika Kanuni ya 2018/848, bali inarejelea taasisi zinazotambuliwa na sheria za kitaifa kuwa na utambulisho wa kipekee pamoja na haki na wajibu wa kisheria; hivyo, zina uwezo wa kutekeleza mambo ya kisheria ambayo mtu binafsi anaweza kuyafanya (k.m. kumiliki mali, kuingia katika mikataba, n.k.) kwa mujibu wa sheria za nchi husika.

Kanuni (EU) Na. 2018/848 haizuii kundi la waendeshaji kushiriki kama wanachama katika aina nyingine za vyama vya wakulima au mifumo mingine, kama vile vyama vya ushirika, mradi tu masharti yote husika yanazingatiwa.

GoO itakuwa chombo cha kisheria kinachotambuliwa na sheria za kitaifa kuwa na haki na wajibu kulingana na sheria ya kitaifa; baadhi ya aina za kisheria zinaweza kutambuliwa bila usajili

Chombo cha kisheria cha GoO kinaweza kuwa mwanachama wa shirika jingine au kuwa na wajibu wa kimkataba na wa ushirikiano na chombo kingine. Hili siyo jambo linalohitajika wala halijazuiliwa.

Maswali juu ya «Utu wa Kisheria» wa GoO

Ni aina gani ya utambulisho wa kisheria unaokubalika kwa chombo cha kisheria cha kundi la opereta?

Kimsingi, GoO inaweza kuwa aina yoyote ya chombo chenye utambulisho wa kisheria kinachotambuliwa na sheria ya taifa kama chenye haki, wajibu, na utambulisho wa kipekee. Hata hivyo, chombo hicho cha kisheria cha GoO kinapaswa kuundwa na wanachama ambao ni wakulima pekee (au operetai wa shughuli za ufugaji wa viumbe vya majini/mwani).

KUMBUKA: Muundo wa kisheria wa GoO unapaswa kuruhusu kuondoa wanachama kwa urahisi; kwa mfano, iwapo hawakidhi tena vigezo vya kilimo hai au ukubwa wao unazidi kiwango kinachoruhusiwa kuruhusu uidhinishaji wa GoO.

Taasisi mpya ya kisheria ya GoO inaweza kuwa na uhusiano wa kimkataba na taasisi nyingine ya kisheria. Kwa mfano, katika hali ya ushirika yenye wanachama wasio wa kilimohai, taasisi mpya ya GoO inaweza kutambuliwa kisheria kama "Umoja wa wanachama wa ushirika wa kilimohai" ambao wanafanya mauzo kupitia ushirika pekee.



Kikundi kipya = GoO



Mifano ya taasisi za kisheria zinazoundwa na wakulima

- ❖ Chama cha ushirika cha kilimo kilichosajiliwa au aina nyingine ya vyama vya wakulima.
- ❖ Aina yoyote ya chama au shirika (kama vile taasisi, shirika lisilo la kiserikali, kikundi cha kusaidiana, biashara ya kijamii, shirika la kijamii, n.k.) linaloundwa na wakulima kwa lengo la kusaidia wakulima wa kilimo hai na kutafuta masoko kwa ajili ya mazao yao.
- ❖ Makampuni ya wakulima; iliyosajiliwa kwa madhumuni ya biashara ya kuuza kwa pamoja mazao kutoka kwa wakulima wa kilimohai ambao ni wanahisa katika kampuni hiyo.

Vikundi vinaweza kuhitaji ushauri wa kisheria ili kupata mikataba inayofaa ya kisheria na ya kimkataba kulingana na sheria ya kitaifa.



“Ukaribu wa kijiografia.”

Ibara ya 36.1.(e): “GoO itaundwa tu na wanachama ambao shughuli zao za uzalishaji (...) zinafanyika katika maeneo yaliyo karibu kijiografia ndani ya Nchi Mwanachama au ndani ya nchi ya tatu”

GoO



Je, kuna mahitaji mapya ya kina kuhusu «ukaribu wa kijiografia»?

“Sharti la “ukaribu wa kijiografia” limekuwepo kwa ajili ya uthibitishaji wa kikundi kwa zaidi ya miaka 20. Kanuni mpya ya Umoja wa Ulaya (EU) haijaweka vigezo vipya mahususi vya kutathmini “ukaribu wa kijiografia” na chombo cha uthibitishaji (CB), isipokuwa sharti la kuwa katika nchi moja.


Ukaribu wa kijiografia ni muhimu sana kwa Mfumo wa Udhibiti wa Ndani (ICS) unaofanya kazi vizuri na kwa ufanisi kutokana na sababu za kiutendaji; hivyo, itabidi wamiliki wa mfumo (GoO) waonyeshe kuwa ICS yao inakidhi mahitaji iwapo wakulima wamepangwa, kwa mfano, katika makundi ya kikanda.

Kumbuka: Miradi mingi iliyoidhinishwa inaweza kuhitaji kupitia upya mfumo wake wa kuwapanga wakulima katika makundi wakati wa kubainisha kundi (au makundi) jipya na halali kisheria la wakulima linalofaa zaidi, ili kukidhi matakwa ya GoO..

Mustakabali wa makundi yanayoongozwa na wasindikaji au wasafirishaji

Kampuni ya usindikaji/usafirishaji bidhaa nje inayoshirikiana na wakulima au kufanya nao kazi kwa mikataba HAIUNDWI NA WAKULIMA na haiwezi kuthibitishwa kuwa GoO. Hii ni nia ya wazi ya watunga sheria wa Ulaya

Itahitajika taasisi moja (au kadhaa) ya kisheria ili kuthibitishwa kama GoO; kila moja ikiwa na hadhi yake binafsi ya kisheria na kuundwa na wakulima wadogo pekee wanaozalisha kwa njia ya kilimohai au walio katika kipindi cha mpito kuelekea uzalishaji wa kilimohai.



Je, Muungano wa Ushirika unaweza kuthibitishwa kama GoO?


Vyama au Mashirika (jamii za wakulima za ngazi ya pili au ya tatu) havina uwezekano wa kukidhi ufafanuzi mpya wa GoO kwa kuwa pia vina wakulima wasio wa kilimo hai kama wanachama wa msingi na/au vina zaidi ya wanachama 2000.“

Muungano unaweza kuthibitishwa kama ‘mwendeshaaji’ anayesambaza bidhaa kutoka kwa taasisi za GoO (mfano, vyama vya msingi vilivyothibitishwa au kundi jipya lililosajiliwa la wanachama wa vyama vya msingi vya kilimo hai pekee)

Kumbuka: Huenda kukawa na ‘vyama’ vinavyokidhi ufafanuzi mpya wa GoO, kwa mfano vyama vidogo vya kilimo hai vinaungana kwa madhumuni ya kuunda kitengo kikubwa cha GoO kulingana na masharti ya EU ya GoO

Mfano wa urekebishaji 1: Uthibitishaji wa vyama vya msingi vilivyo kikamilifu vya kilimo hai kama GoO. Muungano unasaidia GoO kwa huduma za ICS na kusambaza bidhaa za kilimo hai

Mfano wa urekebishaji 2: Muungano unaunda chama kipya kilichosajiliwa kwa ajili ya wanachama wote wanaostahiki wa vyama vya msingi vya kilimo hai kama GoO.



Mahitaji ya ICS kwa Makundi ya Opereta (GoO)



Mahitaji ya ICS



Taratibu Zilizoandikwa k.m. Kusajili na kuidhinisha wanachama wapya wa ICS, ukaguzi wa ICS, hatua zinazochukuliwa kunapokuwa na ukiukwaji.



Meneja na Wakaguzi wa ICS
• Mafunzo ya kila mwaka ya Wakaguzi wa Ndani



Nyaraka na Kumbukumbu za ICS



Ukaguzi wa ndani wa asilimia 100 ya wanachama.



Kusimamia Ukiukaji wa Sheria na kutoa taarifa kwa CB ikiwa wanachama watasimamishwa/kufutiwa a usajili.



Ufuatiliaji na udhibiti wa mtiririko wa bidhaa na rekodi



Mafunzo ya Wakulima (kila mwaka)

Taratibu za ICS.



Taratibu za ICS
zimeandikwa na
kuwekwa katika
"Mwongozo wa
ICS"

ICS itakuwa na taratibu zilizorekodiwa kuhusu:

(i) usajili wa
Kikundi cha
operetta GoO

(ii) UKaguzi
wa ndani wa
wana kikundi
wote.

(iii) Uidhinishaji
wa wanachama
wavya au
vitengo/shighuli
mpya

(iv) Mafunzo
kwa wakaguzi
wa ICS.

(v) Mafunzo
kwa
wanakikundi
wa GoO.

(vi) Udhibiti
wa nyaraka
na rekodi

(vii) Hatua
katika hali ya
kutokufuata
masharti

(viii) Ufuatiliaji
wa ndani wa
bidhaa

Wasimamizi wa ICS na wakaguzi wa ICS.



Jukumu la meneja wa ICS linahitaji nafasi ya ngazi ya juu katika shirika, ikiambatana na mamlaka pamoja na ujuzi wa kiutawala na utaalum wa kusimamia uzingatiaji wa kanuni na taratibu.

Meneja wa ICS" ana jukumu la:

- i. Kuthibitisha ustahiki na kuidhinisha wanachama wa GoO, vitengo vipya, n.k.
- ii. Kuhakikisha kwamba kuna mkataba kwa kila mwanachama
- iii. Kuandaa na kutunza orodha ya wanachama
- iv. Kuandaa taratibu na fomu za ICS; kuhakikisha rekodi zimesasishwa
- v. Kugawa kazi na majukumu kwa wakaguzi wa ICS na kupanga ratiba ya ukaguzi wa ndani na kuhakikisha unatekelezwa kikamilifu

Kundi la operetta (GoO) linaweza 'kuteua' msimamizi wa ICS wa nje.

Mtu mmoja hawezi kujumuisha wajibu wa msimamizi wa ICS na mkaguzi wa ICS

Wasimamizi wa ICS na wakaguzi wa ICS.



GoO inahitaji kuteua idadi ya kutosha ya wakaguzi wa ICS wenye uwezo kwa ajili ya ukaguzi wa kila mwaka wa wanachama. Kufanya mafunzo ya kila mwaka pamoja na tathmini ya maarifa yaliyopatikana. Kuwasilisha na kusasisha tamko kuhusu mgongano wa maslahi kila mwaka.

Meneja wa ICS" ana jukumu la:...

- vi. Kuwa kiungo na CB; kuamua na kufanya mawasiliano na CB
- vii. Kuhakikisha mafunzo ya kila mwaka ya wakaguzi wa ICS na kufanya tathmini ya uwezo na mafunzo yanayotolewa kwa wanachama
- viii. Kuamua hatua za kuchukuliwa iwapo kutatokea ukiukwaji wa sharia, kanuni na masharti.
- ix. Kuamua na kusaini makubaliano ya shughuli za mikataba midogo

Nyaraka na Rekodi za ICS za Lazima.



I. Orodha ya wanachama

- II. Mikataba ya “uanachama” iliyotiwa saini (Ibara ya 36.1 (g))
- III. Ripoti za ukaguzi wa ndani
- IV. Rekodi za mafunzo na migongano ya kimaslahi ya wakaguzi wa ICS
- V. Rekodi za mafunzo ya wanachama
- VI. Hatua zilizochukuliwa iwapo kutakuwa na ukiukaji wa kanuni
- VII. Rekodi za ufuatiliaji wa historia ya bidhaa (traceability)
- VIII. Mikataba ya ukandarasi mdogo
- IX. Uteuzi wa Meneja wa ICS na Wakaguzi wa Ndani

Orodha ya lazima ya wanachama

(Tarehe & Toleo)

Jina la mkulima, utambulisho, mawasiliano

Tarehe au usajili

Jumla ya eneo la ardhi linalosimamiwa na mwanachama, na iwapo ni sehemu ya kitengo cha uzalishaji wa kilimohai, cha mpito, au kisicho cha kilimohai.

Taarifa kuhusu kila kitengo cha uzalishaji:
ukubwa, mahali*, mazao, muda wa kuanza
kipindi cha mabadiliko, makadirio ya mavuno.

Nyaraka na Rekodi za ICS za Lazima .



I. Orodha ya wanachama

II. Mikataba ya “uanachama” iliyotiwa saini (Ibara ya 36.1 (g))

III. Ripoti za ukaguzi wa ndani

IV. Rekodi za mafunzo na migongano ya kimaslahi ya wakaguzi wa ICS

V. Rekodi za mafunzo ya wanachama

VI. Hatua zilizochukuliwa iwapo kutakuwa na ukiukaji wa kanuni

VII. Rekodi za ufuatiliaji wa historia ya bidhaa (traceability)

VIII. Mikataba ya ukandarasi mdogo

IX. Uteuzi wa Meneja wa ICS na Wakaguzi wa Ndan

Wajibu wa Wanachama (minimal)

Kuzingatia Kanuni za Umoja wa Ulaya (EU)

Kushiriki na kushirikiana na ICS, ikiwemo utunzaji wa kumbukumbu

Kuwaruhusu Wakaguzi wa ndani na nje kufanya ukaguzi

Kukubali kuchukua hatua za kurekebisha ukiukwaji wa sharia, kanuni.

Toa taarifa mara moja kwa Meneja wa ICS iwapo kuna mashaka ya ukiukwaji

Nyaraka na rekodi za lazima za ICS.



- I. Orodha ya wanachama
- II. Mikataba ya “uanachama” iliyotiwa saina (Ibara ya 36.1 (g))
- III. Ripoti za ukaguzi wa ndani**
- IV. Rekodi za mafunzo na migongano ya kimaslahi ya wakaguzi wa ICS
- V. Rekodi za mafunzo ya wanachama
- VI. Hatua zilizochukuliwa iwapo kutakuwa na ukiukaji wa kanuni
- VII. Rekodi za ufuatiliaji wa historia ya bidhaa (traceability)
- VIII. Mikataba ya ukandarasi mdogo
- IX. Uteuzi wa Meneja wa ICS na Wakaguzi wa Ndan

Taarifa za Ukaguzi wa Ndani (kwa ufupi) (zilizosainiwa na Mkaguzi wa ICS na Mwanachama. signed by ICS inspector and member)

Jina la mwanachama na maeneo ya vitengo au majengo ya uzalishaji, ikijumuisha vituo vya ununuzi na ukusanyaji vinavyofanyiwa ukaguzi.

Tarehe na saa ya kuanza na kumaliza

Upeo wa ukaguzi (mipaka)

Tarehe ya kutoa ripoti

Jina la Mkaguzi wa ICS

Maelezo ya ukiukwaji uliobainishwa

Nyaraka na rekodi za lazima za ICS.



- I. Orodha ya wanachama
- II. Mikataba ya “uanachama” iliyotiwa saini (Ibara ya 36.1 (g))
- III. Ripoti za ukaguzi wa ndani
- IV. Rekodi za mafunzo na migongano ya kimaslahi ya wakaguzi wa ICS
- V. Rekodi za mafunzo ya wanachama**
- VI. Hatua zilizochukuliwa iwapo kutakuwa na ukiukaji wa kanuni
- VII. Rekodi za ufuatiliaji wa historia ya bidhaa (traceability)
- VIII. Mikataba ya ukandarasi mdogo
- IX. Uteuzi wa Meneja wa ICS na Wakaguzi wa Ndan

Taarifa fupi

Tarehe

Mada

Mkufunzi

Tathmini ya maarifa yaliyopatikana (pale inapofaa)

Taarifa fupi

Nyaraka na rekodi za lazima za ICS.



- I. Orodha ya wanachama
- II. Mikataba ya “uanachama” iliyotiwa saini (Ibara ya 36.1 (g))
- III. Ripoti za ukaguzi wa ndani
- IV. Rekodi za mafunzo na migongano ya kimaslahi ya wakaguzi wa ICS
- V. Rekodi za mafunzo ya wanachama
- VI. Hatua zilizochukuliwa iwapo kutakuwa na ukiukaji wa kanuni**
- VII. Rekodi za ufuatiliaji wa historia ya bidhaa (traceability)
- VIII. Mikataba ya ukandarasi mdogo
- IX. Uteuzi



Maelezo Mafupi

Utambulisho wa mwanachama anayehusika na hatua hizo iwapo kutakuwa na kutotii: kusimamishwa, kuondolewa au kutakiwa kufuata kipindi kipya cha mabadiliko/mpito.

Maelezo ya Mapungu/ukiukwaji uliobainishwa

Maelezo ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa kurekebisha kasoro zilizojitokeza

Maelezo Mafupi

Utambulisho wa mwanachama anayehusika na hatua hizo iwapo kutakuwa na kutotii: kusimamishwa, kuondolewa au kutakiwa kufuata kipindi kipya cha mabadiliko/mpito.

Nyaraka na rekodi za lazima za ICS.



- I. Orodha ya wanachama
- II. Mikataba ya “uanachama” iliyotiwa saina (Ibara ya 36.1 (g))
- III. Ripoti za ukaguzi wa ndani
- IV. Rekodi za mafunzo na migongano ya kimaslahi ya wakaguzi wa ICS
- V. Rekodi za mafunzo ya wanachama
- VI. Hatua zilizochukuliwa iwapo kutakuwa na ukiukaji wa kanuni
- VII. Rekodi za ufuatiliaji wa ya bidhaa (traceability) historia**
- VIII. Mikataba ya ukandarasi mdogo
- IX. Uteuzi

Maelezo kwa ufupi (1)

Ununuzi na usambazaji wa pembejeo za kilimo

Rekodi za mavuno na nyinginezo zinazohusiana na shamba

Rekodi zinazohusiana na uhifadhi wa bidhaa

Rekodi zinazohusiana na utayarishaji wa bidhaa

Rekodi zinazohusiana na uwasilishaji wa bidhaa kwa kila mwanachama na JMS

Mauzo ya bidhaa za kundi

Mahitaji ya msingi (2)

Jinan a anuani ya wasambazaji

Jina na anwani ya mpokeaji, mnunuzi au mwagizaji

Cheti cha msambazaji

Nyaraka zinazohusiana na usafirishaji wa bidhaa

Taarifa za utambulisho wa mzigo/fungu

Kwa wasindikaji: taarifa zote zinazohitajika ili kuwezesha mchakato wa ufuatiliaji

Wakaguzi wa ndani wa ICS.

ICS inapaswa kufanya ukaguzi wa wanachama wote (asilimia 100) kila mwaka. Tarehe ya ukaguzi wa ICS inahitaji kuonyeshwa kwenye orodha ya wanachama



ya shambani kwa kitengo cha kilimo hai na cha uongofu (mazao yote), ukaguzi wa ghafla wa kitengo kisicho cha kilimo hai.

Mahojiano ya Mkulima

Taarifa za shambani za ziko sahihi?

Makadirio ya Mavuno

**Ukaguzi
vya ICS**

"Matumizi na uhifadhi wa viingilio


*Utambuzi wa hatari;
kuepuka uchafuzi*

*Maandalizi baada ya mavuno
na uhifadhi wa bidhaa*

ICS itatumia mbinu inayozingatia hatari:
Ukaguzi unapaswa kufanyika nyakati tofauti ili
kushughulikia hatari katika kipindi chote cha uzalishaji!



Uidhinishaji wa ICS na Usimamizi wa hali ya ukiukwaji wa masharti.



Rekodi za hatua zilizochukuliwa na meneja wa ICS iwapo kutakuwa na ukiukwaji wa kanuni.

I. Wanachama wanaokabiliwa na adhabu, ni pamoja na wale waliosimamishwa, walioondolewa au wanaohitajika kupitia upya katika kipindi cha mpito.

II. Maelezo ya ukiukwaji sheria na kanuni uliobainishwa.

III. Maelezo ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa, k.m. taarifa kwa mwanachama; taarifa kwa kituo cha ununuzi; taarifa kwa CB ikiwa inahitajika, mafunzo ya wanachama, ziara za mara kwa mara za ICS.

Taarifa za Meneja wa ICS iwapo kutatokea ukiukwaji mkubwa wa sharia na kanuni
Meneja wa ICS atajulisha mara moja chombo cha udhibiti kuhusu (a) kunapokuwa na shaka yoyote ya ukiukwaji wa kanuni kwa kiwango kikubwa; (b) kusimamishwa au kuondolewa kutoka kwenye kundi kwa mwanachama, kitengo cha uzalishaji, au eneo lolote (ikiwemo vituo vya ununuzi na ukusanyaji); (c) marufuku yoyote ya kuingiza sokoni fungu fulani la bidhaa likiwa na lebo ya "kilimohai".

Makundi Mapya ya EU ya Kutokufuata Masharti

Kutokufuata Masharti Madogo

Kutokufuata Masharti Makubwa

Kutokufuata Masharti Makubwa na ya Msingi

Katalogi ya hatua kwa haya makundi 3 ya kutokufuata masharti

Mafunzo na msaada kwa Wakulima



Mafunzo bora na kuwasaidia wakulima ni muhimu katika uzalishaji wa kilimohai. Shughuli za kivitendo shambani na ufafanuzi wa kanuni za uzalishaji kwa kutumia mifano ya moja kwa moja shambani ndiyo njia inayofaa zaidi.

Mafunzo kwa wakulima kama sharti jipya la EU


I. ICS itakuwa na utaratibu wa “kuwapa mafunzo wanachama wa GoO kuhusu taratibu za ICS na mahitaji ya Kanuni ya EU kuhusu kilimohai”.

II. Mafunzo kwa wanachama yatarekodiwa.

’
.



Ufuatiliaji na Udhhibiti wa Mtiririko wa Bidhaa



ICS itajumuisha taratibu zilizowekwa kuhusu ufuatiliaji wa ndani, ambazo:

- zinaonyesha asili ya bidhaa katika mfumo wa pamoja wa masoko na
- zinawezesha kufuatilia bidhaa zote za wanachama katika hatua zote, kama vile uzalishaji, uchakataji, uandaaji au usafirishaji kwenda nje ya nchi
- zinajumuisha makadirio na uhakiki wa kiasi cha mavuno ya kila mwanachama”

Kumbuka: mahitaji mapya yanapanua wajibu wa ICS, zaidi ya kuwasilisha bidhaa kwenye vituo vya ununuzi – ICS inawajibika kufanya ufuatiliaji hadi hatua ya mauzo yanayofanywa na taasisi ya kisheria ya GoO.

Kumbuka: mahitaji mapya yanaongeza wajibu wa ICS zaidi ya usafirishaji hadi vituo vya ununuzi – ICS inawajibika kwa ufuatiliaji hadi mauzo yanapofanywa na taasisi ya kisheria ya GoO

Wakati wa ununuzi, kiasi kilichopokelewa kutoka kwa wanachama lazima kijumlishwe na kilinganishwe na makadirio ya mavuno.

Ni muhimu kuwepo mfumo thabiti wa kutambua mafungu ya bidhaa, kuanzia hatua ya ununuzi, maandalizi na uhifadhi, hadi uuzaji wa mwisho



Kumbuka: Iwapo kutatokea ukiukwaji mkubwa, hatua kali zaidi zitachukuliwa ikiwa mafungu husika hayatapatikana.

Rekodi za ufuatiliaji

Ununuzi na usambazaji wa pamoja wa pembejeo za kilimo

I. Rekodi za uwasilishaji wa bidhaa kutoka kwa kila mwanachama

II. Rekodi za uzalishaji, uhifadhi (uingizaji na utoaji) na uandaaji wa GoO

III. Mauzo ya bidhaa yaliyofanywa na GoO

Ufuatiliaji na Udhibiti wa Mtiririko wa Bidhaa.

Ufuatiliaji na Udhibiti wa Mtiririko wa Bidhaa

Ufuatiliaji kamili wa ndani—kuanzia kwa wakulima wa kilimo hai hadi hatua ya mauzo yanayofanywa na Kundi—ni jukumu la msingi la ICS na una umuhimu mkubwa katika kuhakikisha ubora na uhalisi wa bidhaa za kilimo hai. Ikumbukwe kuwa ICS itawajibika kusimamia ufuatiliaji huo katika hatua zote (hata baada ya ununuzi) hadi pale mauzo yatakapofanywa na GoO!



ICS inapaswa kukagua kwa ndani vituo vyote vya ununuzi kila mwaka

Mfumo wa ndani wa kufuatilia bidhaa unaoruhusu kufuatilia bidhaa zote za wanachama wa GoO katika hatua zote, hadi kufikia hatua ya mauzo yanayofanywa na GoO.

EU inaweza kuomba kufuatilia kundi la bidhaa (lot) hadi kwenye shamba asili.

(GoO lazima itunze) Kumbukumbu za uwasilishaji wa bidhaa kutoka kwa kila mwanachama kwenda kwenye mfumo wa pamoja wa masoko.

Matarajio makubwa ya ufuatiliaji wa bidhaa ni kuwa, kwa kila kundi la bidhaa, ni lazima kurekodi wanachama waliochangia pamoja na kiasi walichotoa.

Kanuni kuu za maandilizi au uchakataji unaofanywa na wanakikundi.

Mara nyingi, wanachama wa GoO hujihusisha na shughuli za kuchakata na kuhifadhi mazao ya kilimohai kabla ya kuyauza kupitia mfumo wa pamoja wa masoko wa GoO. Shughuli hii lazima idhibitiwe na ICS!



Kanuni kuu za uzalishaji kwa wanakikundi.

Hatua za tahadhari ili kuepuka kuchanganyika na uchafuzi wa bidhaa iliyothibitishwa katika hatua zote:

- Wakati mwanachama anapofanya shughuli zote za baada ya mavuno
- Wakati wa kuhifadhi shambani
- Wakati mwanachama anasafirisha bidhaa kwenda kituo cha ununuzi
Kumbuka: hatua zinazohitajika za utenganishaji ikiwa mwanachama anashughulikia zao moja katika ubora wa kilimohai/ kipindi cha mpito ni ngumu kusimamia katika GoO - inawezekana chini ya usimamizi wa ICS wa mavuno na uchakataji wa mwanachama;
- Bidhaa zilizotambuliwa pekee ndizo zitakazoruhusiwa kusafishwa na kudhibiti wadudu waharibifu katika eneo la uzalishaji, usindikaji na uhifadhi shambani kuanzia 2024
- Vitu vilivyoidhinishwa pekee vinaweza kutumika wakati wowote kudhibiti wadudu katika eneo lolote ambapo bidhaa za kilimohai huhifadhiwa au kushughulikiwa

Ununuzi, usafirishaji, uhifadhi, na maandalizi kwenye GoO.



Kanuni za Jumla za Ukusanyaji zinazotumika kwa GoO

Iwapo wakulima watakabidhi bidhaa kwenye kituo cha ununuzi cha GoO

Risiti kwa mkulima na rekodi ya ununuzi

Ukaguzi wa mapokezi ulioandikwa: hali ya uthibitisho wa mwanachama na makadirio ya mavuno



Iwapo mfumo wa ukusanyaji wa mazao shambani unatumika na GoO: Hatua za kina zinazopaswa kuchukuliwa na dereva wa ukusanyaji : Kiambatisho III. /

Kanuni za jumla za uhifadhi na kuandaa bidhaa za kilimo hai wakati wote

- **Uhifadhi:** Utambuzi wa wazi wa bidhaa za kilimohai wakati wowote, na hatua za kina iwapo kutahifadhiwa bidhaa za viwango mbalimbali vya ubora au bidhaa nyingine za kilimo.
- **Hatua za tahadhari kuepuka uchafuzi na kuchanganyikana** (maeneo safi ya ufungashaji na uhifadhi, yaliyoidhinishwa pekee kwa ajili ya kudhibiti wadudu katika maeneo yanayotumika kuhifadhi bidhaa za kilimohai wakati wowote, n.k.)



Iwapo GoO itachakata bidhaa za wanachama (mfano: uchimbaji, ukavuaji).

HITIMISHO

- Seti hii imeangazia viashiria vya msingi vya mfumo wa ICS na mahitaji ya viwango vya kilimohai vya Ulaya katika uzalishaji. Mada hii ni muhimu ili kujenga ICS imara na yenye manufaa kwa wazalishaji na walaji wa bidhaa za kilimohai.
- Katika Seti ya siku ya pili utajifunza zaidi kuhusu mahitaji ya viwango vya kilimohai vya ulaya kwa vikundi vya wakulima na opereta wengine.

Imeandaliwa na Shirika Mwamvuli la Kilimohai Tanzania (TOAM) kupitia mradi wa kitovu cha maarifa Afrika Mashariki (Knowledge Hub for Organic Agriculture and Agroecology Tanzania - KHEA)

Kupata seti ya siku ya pili na ya tatu tembelea jukwaa la kidijitali la maarifa ya kilimohai na kilimoikolojia katika tovuti: <https://khea-africa.org/>


Tunapatikana:

Mtaa wa Samora Avenue, Jengo la Kelvin House, gorofa ya Kwanza.

Kwa mawasiliano Zaidi tupigie kupitia +25574413499



Asante sana na karibu uendelee na seti ya siku ya tatu



In cooperation with

